UTANGULIZI KWA ELIMU
YA KIFEDHA

MAELEZO SAHIHI

KUTAFSIRI ELIMU YA KIFEDHA

- Fedha ni kuhusu jinsi unavyopata na kusimamia pesa zako
- Pesa ni rasilimali ambayo watu wanahitaji kwa ustawi wao. Pesa huwezesha upatikanaji wa chakula, mavazi, makao, na elimu. Pesa pia huwezesha kupanga kwa ajili ya siku zijazo, na kuishi maisha yenye afya na tija.
- Elimu ya kifedha ni ujuzi na maarifa ambao watu wanaweza kujifunza ili kusimamia pesa zao na kujijengea mali, kuelewa jinsi pesa inavyofanya kazi katika jumuiya yako, na kufanya maamuzi mazuri ya nini cha kufanya na pesa zako.
- Mali ni vitu ambazo zina thamani ya kifedha. Mali inaweza kuwa ardhi, magari, mashine, majengo
- Pesa inapita kwa njia tofauti tofauti. Hizi ni baadhi ya njia ambazo pesa hupatikana na kubadilishanwa katika jumuiya:



Kukopa inamaanisha kuchukua pesa ambayo si yako kwa kuazima. Hii ina maana kwamba mtu anakubali kukukopesha pesa, na wewe unakubali kuirejesha. Unaweza kukopa fedha kutoka benki, au kwa jirani. Mara nyingi unapaswa kulipa riba kwa matumizi ya pesa ulizokopa. Unapochukua muda mrefu kulipa mkopo, riba inaongezeka, na gharama ya mkopo kuwa ghali zaidi kwako.

Riba ni gharama ya unayotozwa kwa kukopa pesa. Kwa mfano, unaweza kutozwa kiwango cha riba kwa pesa ulizokopa. Hii inamaanisha kuwa utalipa asilimia ya kiasi kile cha pesa ambacho bado unadaiwa katika mkopo, kwa kawaida huwa ni kila mwisho wa mwezi.

Kuweka akiba (kutunza pesa) humaanisha kutotumia pesa zote abazo unazopata, ila kuweka kiasi fulani kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Kutenga kiasi kidogo cha pesa mara kwa mara ni njia nzuri ya kutunza mahitaji yako ya baadaye. Zaidi unavyo weka pesa kwenye akiba, utaweza kuwa na pesa za kutosha kuanzisha biashara yako, au kushughulikia gharama za matibabu ya kiafya katika familia.



Uwekezaji ni kuweka pesa katika kuendeleza kitu ambacho unatarajia kitakuleta mapato siku zijazo. Kwa mfano, unaweza kuwekeza pesa kwa kuanzisha biashara, au kuendeleza elimu yako ili kuboresha mapato yako ili kupata mapato zaidi.

"Elimu ya kifedha humaanisha kuwa na maarifa na ujuzi wa kufanya maamuzi mazuri kuhusu jinsi unavyopata, kutumia, kukopa, kuweka akiba na kuwekeza pesa zako. Maamuzi mazuri ya kifedha yanaweza kusaidia kuboresha ustawi wako na ubora wa maisha"

(Mastercard, Taking Stock)

PESA: JINSI PESA HUZUNGUKA: NJIA RASMI NA ZISIZO RASMI

- Pesa huzunguka katika njia mbali mbali ikiwa ni pamoja na kubadilishwa katika sekta rasmi na sekta isiyo rasmi.
- Sekta rasmi inajumuisha mabenki na biashara zilizosajiliwa na kuwa kwenye taratibu pamoja na kutozwa kodi (ushuru).
- Shughuli zote za kiuchumi zilizo nje ya utaratibu na ulipwaji kodi huhesabiwa kuwa ni shughuli ambazo ziko kwenye uchumi usio rasmi.
- Sekta rasmi na zisizo rasmi hutegemeana, lakini kuna mgawanyiko mkubwa kati yake. Kwa mfano, watu wanaofanya kazi katika sekta isiyo rasmi hawawezi kupata bidhaa rasmi za kifedha, kama akaunti ya benki.
- Kupata bidhaa na huduma zinazotolewa na mabenki na taasisi nyingine rasmi zinaweza kuwa changamoto kubwa kwa watu ambao hawana kazi rasmi(ajira), au kwa watu ambao hawawezi kutoa hati rasmi kama hati ya nyumba.
- Shughuli nyingi za kiuchumi nchini Tanzania hufanyika katika sekta isiyo rasmi. Shughuli za kiuchumi zisizo rasmi zinajumuisha uchuuzi mitaani au sokoni, kutoa bidhaa na huduma kama vile kushona nguo, kazi zisizolipwa kwenye mashamba ya familia, na kazi za nyumbani kama vile kupika, kusafisha na kutunza watoto.
- Kuna uwezekano mkubwa zaidi kupata wanawake wengi kuliko wanaume wakifanya kazi katika sekta isiyo rasmi, na pia kuna uwezekano mkubwa kuwa wao hawalipwi chochote au wanalipwa kidogo sana kwa kazi wanazofanya.

JE, WAJUA?



NI VIJANA 4% TU YA VIJANA NCHINI TANZANIA (WENYE UMRI WA MIAKA 15-24) AMABO WANA AKAUNTI YA BENKI. 64% YA VIJANA WAKITANZANIA HAWANA AKAUNTI YA BENKI WALA AKAUNTI INAYOTUMIKA YA MPESA KWENYE SIMU ZAO

(Youthstart 2016)

AJIRA NI SABABU KUBWA INAYOATHIRI UPATIKANAJI WA FEDHA KWA VIJANA. NCHINI TANZANIA, VIJANA WASIO NA AJIIRA NI MARA MBILI YA KIWANGO CHA WATU WAZIMA

(Youthmap Tanzania)

NI 5.7% TU YA VIJANA 800,000 WA TANZANIA WANAOINGIA KATIKA SOKO LA AJIRA HUFANIKIWA KUPATA AJIRA RASMI KILA MWAKA

(Vijana wa 2016)

Idadi ya wanawake wasio na ajira nchini Tanzania imezidi ya wanaume kwa asiiimia 33%

(Restless Development 2011)

TAKRIBAN 80% YA WATANZANIA WANATUNZA PESA. WENGI WAO WANAPENDELEA KUWEKA AKIBA ZAO NYUMBANI (70%). NI 13% TU YA WATU WANAOPENDELEA KUWEKA AKIBA YA PESA ZAO KWENYE BENKI



(Intermedia 2014)

JE, WAJUA?

Vijana Watanzania hawaziamini na pia hawafikiwi na huduma za mikopo, kwa hiyo wanapendelea kukopa pesa kutoka kwa familia, marafiki na vyanzo vingineo visivyo rasmi



(Youthstrart 2016)

VIJANA WAMERIPOTIWA KULIPIA RIBA HADI KIASI

CHA 300% KUTOKANA

NA MIKOPO WALIYOPATA KUTOKA VYANZO VISIVYO RASMI

(Vijana wa 2016)

KUELEWA KUJUMUISHWA KIFEDHA

- Kujumuishwa kifedha kunamaanisha sio kuwa tu na ujuzi kuhusu jinsi pesa zinavyofanya kazi, lakini pia kuwa na rasilimali muhimu na fursa za kushiriki katika mfumo wa pesa. Ndiyo maana ni muhimu kuelewa ni nani aliyejumuishwa na ambaye ametengwa katika mfumo wa pesa wa jumuiya yako, na ni kwa sababu gani.
- Hebu fikiria nguzo nne za kujumuishwa kifedha: sera, upatikanaji, uwezo wa kununua na elimu:
  - **Sera** ndio hufungua au kufunga milango ya wewe kujumuishwa katika mambo ya kifedha ya jumuiya na nchi yako
  - Sera ya Taifa ya Vijana inatambua changamoto za ajira zinazokabiliwa na vijana, na inataka kukuza ujasiriamali na ajira binafsi kama njia mbadala kwa vijana (Youthstart 2016)
  - Sera zingine zinazohusiana na fedha kama vile Mkakati wa Taifa wa Ujumuishaji Kifedha zinazingatiwa kuwa za maendeleo, lakini hazijaenezwa vya kutosha ili kuleta utofauti katika maisha ya vijana walio wengi nchini.
  - Maswali ya Sera: Je, unonaje sera za kifedha zinavyoakisi katika maisha yako? Na kwa maisha ya jumuiya yako?
  - **Uwezo wa kumudu:** Watu wanahitaji kuwa na uwezo wa **kumudu** bidhaa za kifedha na jinsi ya kubadilishana. Mara nyingi kuna gharama za kuzingatia, kwa mfano ada za malipo na riba, zinazohusishwa na akaunti ya benki, kuchukua mkopo, au kukopa kutoka kwa rafiki
  - Kuna gharama zilizofichika pia. Gharama zilizofichika inajumuisha muda, gharama za kifedha na kifursa ambazo zinakugharimu kusafiri kwenda tawi la benki ambalo liko mbali, ikiwa unaishi katika kijijii.
  - Maswali ya uwezo wa kumudu: Maisha yako na ya jamii yako yanaathirika vipi kutokana na gharama za huduma za kifedha, kwa mfano kumudu gharama za kuchukua mkopo?
  - **Elimu:** watu pia wanapaswa kuelewa bidhaa mbalimbali za kifedha ambazo zinapatikana, na kuamua kama bidhaa hizo zina manufaa kwao. Elimu ya kifedha husaidia kukuza mikakati mizuri ya kukopa, kuweka akiba na kuwekeza pesa
  - Mabenki, tasasi zisizo za serikali na mashirika mengine yanazidi kutoa elimu ya kifedha ambayo ina lengo la kuwasaidia wateja na wanaotazamiwa kuwa wateja kufanya maamuzi bora ya kifedha
  - Maswali kuhusu elimu ya kifedha: Je, wewe unajielimisha vipi juu ya bidhaa za kifedha zilizo katika jamii yako? Nini rasilimali zipi zinazopatikana katika jumuiya yako ya kujifunza kuhusu fedha?
- **Upatikanaji:** inahusiana na uwezekano wa kufikia na

KUELEWA KUJUMUISHWA KIFEDHA

kushirikiana na rasilimali mbalimbali za kifedha katika jumuiya yako

- Upatikanaji unaathiriwa na vitu kama unapoishi, umri wako, jinsia, kiwango cha elimu, na matarajio ya mapato au ajira.
- Upatikanaji pia unaweza kuathiriwa na mila za jinsia. Kwa mfano, wanaume wengi, kuliko wanawake, wana elimu ya sekondari na hivyo kuwawezesha wanaume kuzipata huduma za kifedha kwa urahisi. (UNESCO)
- Teknolojia na miundombinu pia inaweza kuzuia au kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha. (Money Money)
- Maswali yanayogusia upatikanaji (access): Je, wewe unaonaje mzunguko wa pesa katika jamii yako? Ni bidhaa na huduma zipi za kifedha zinapatikana kwako wewe? Hali yako ya maisha inachangiwa vipi unapozichagua bidhaa au huduma hizo za kifedha? Ufikiaji wako wa rasilimali za kifedha unatofautianaje na wa mtu mwingine?

ZAIDI YA 90% YA VIJANA NCHINI TANZANIA HAWANA AKAUNTI YA BENKI. ZIFUATAZO NI SABABU SITA ZINAZOELEZA NI KWA NINI:

- **Ajira:** Kiwango cha ajira rasmi kwa vijana kiko chini, na mabenki mara nyingi hayashughulikii watu wasio na ajira rasmi.
- **Umaskini:** Mara nyingi vijana hawapati fursa za kazi za kulipwa, hasa katika maeneo ya vijijini, hii inamaanisha kwamba hao vijana basi hawana uwezo wa kuweka akiba ya pesa (Restless Development)
- **Upatikanaji vijijini:** Idadi kubwa ya vijana Tanzania (60%) huishi vijijini, ambako hali ya mtandao wa mabarabara na umeme ni duni, na mabenki ziko mbali kufikika (Youthstart 2016)
- **Elimu:** 21% ya wanaume na 33% ya wanawake hawana elimu ya msingi, hii inamaanisha uwezo wao wa kujihusisha na mabenki na taasisi za fedha ni mdogo (UNESCO)
- **Kujitegemea:** Mara nyingi, vijana wanatarajiwa kupeana mapato yao kwa wakuu wao, hasa mapato yatokanayo na kazi ya kilimo (Youthstart 2016)
- **Uaminifu:** Vijana wengi hawana ufahamu na huduma za kibenki na hawaamini benki kama sehemu sahihi ya kutunzia pesa zao

KUKUSANYA MAARIFA YA FEDHA KATIKA JUMUIYA YAKO. HAYA NI BAADHI YA MASWALI YA KUZINGATIA:

- **Kuweka malengo ya kifedha:** Je, vijana katika jamii yako wana matarajio gani ya kifedha? Je, watu hupanga malengo yao ya kifedha? Ni malengo gani ambayo ni ya muhimu kwa watu? Ni nini kinachofanya watu kujisikia wanaweza kufanikiwa (au kutofanikiwa) kufikia malengo yao ya kifedha?
- **Kukopa** inahusisha makubaliano kati ya mkopaji na mkopeshaji. Wote, akopaye na mkopeshaji, wanahitajika kuelewa makubaliano yao vizuri. Kwa mfano, mkopeshaji anajuaje kwamba akopaye ataweza kulipa mkopo? Je, watu hukopa kwa kutumia mali nyingine walizo nazo? Watu wanafikiaje makubaliano ya mikopo katika jumuiya yako? Je, watu hukopeshana katika familia? Ni nini hufanya watu kuaminiana kwa makubaliano yao? Ni nini hufanyika ikiwa akopaye hata lipa pesa alizokopeshwa?
- **Kuweka akiba** inahusu kutunza pesa ili zikusanyike nyingi. Je, watu hutunzaje pesa katika jumuiya yako? Ni nini huchochea watu kuweka akiba? Wanaweka akiba zao wapi? Katika benki? Akaunti ya pesa kwenye simu? Makundi ya akiba ya jumuiya? Chini ya godoro? Kwenye vitu vyenye thamani? Je, watu huweka akiba kibinafsi au kifamilia? Watu hutumiaje akiba zao? Ni nani anayeamua?

PATA UKWELI! ONDOA UPOTOSHAJI!

UPOTOSHAJI	UKWELI
Unahitaji elimu rasmi ili kuwa na uelewa mzuri wa kifedha	Mtu yeyote anaweza kujifunza kwafanya bajeti, kuweka akiba, kupanga mpango wa baadaye na kufanya maamuzi mazuri ya uwekezaji
Unahitaji pesa nyingi ili kuanzisha biashara yako mwenyewe	Vijana wengi huendesha biashara zao ndogo kama njia yao ya kutimizia mahitaji yao. Wale ambao hufanikiwa katika kukuza biashara zao na kuboresha hali yao ya kifedha huwa ni wale ambao wanaweza kukopa kwa busara na kuchukua tahadhari zilizohesabiwa. Ujuzi huu muhimu unapatikana kupitia elimu ya kifedha Chanzo: Invisible lives
Vijana hawana fursa za kupata huduma za benki na bidhaa za kifedha	Vijana wanakabiliwa na changamoto kubwa za kifedha ambazo zinaendana na chanagamoto za kiajira. Huduma za kifedha kupitia kwenye simu (Mobile Money) zinabadilisha hali ya mambo, hasa kwa watu maskini vijijini. Asilimia 4% tu ya vijana Tanzania wana akaunti ya kibenki. Watu sita kati ya watu 10 Tanzania sasa wana akaunti ya simu Chanzo: InterMedia 2016

NI NINI UHUSIANO KATI YA KUJUMUISHWA KIFEDHA NA AJIRA KWA VIJANA?

- Mwaka 2015, mmoja kati ya vijana watatu duniani atakuwa Mwafrika (UN World Population, 2014). Ifikapo mwaka wa 2030, bara la Afrika linatarajiwa kuwa na idadi kubwa ya nguvukazi, kwa zaidi ya kiasi cha idadi ya vijana milioni 375 (World Bank)
- Vijana nchini Tanzania ni takribani theluthi mbili ya idadi ya watu, lakini kiwango cha kujumuishwa kwao kifedha imebaki kuwa chini (Restless Development)
- Hii inamaanisha kwamba Waafrika sasa wana uwezo wa kusaidia kuunda mwelekeo wa kazi za siku za usoni, lakini vijana hawawezi kutambua uwezo huu wao mkubwa bila kuwezeshwa kifedha
- Idadi ya vijana wa Tanzania inakua kwa kasi zaidi kuliko hapo awali. Uchumi unakua pia (ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 7 kwa mwaka)
- Lakini si kwa haraka sanjali na ukuaji wa idadi ya watu.
- Ukuaji wa kiuchumi haujajumuisha vijana, na pengo la ajira kwa vijana Tanzania linazidi kupanuka (Youthstart 2016)
- Kwasababu kuna upungufu wa ulinzi wa kijamii vijana wengi hawawezi kustahimili kukaa bila ajira. Fursa za ajira rasmi ni chache, na vijana wengi hutegemea kujihushisa na shughuli tofauti tofauti ili kutimiza mahitaji yao (Invisible Lives)
- Watunga sera na sekta ya kifedha wanatambua umuhimu wa kuongeza na kueneza maarifa ya kifedha kwa vijana na kuwahusisha vijana katika masuala ya kifedha (Youthstart 2016).

JINSIA

- Vijana wa kike wanakabiliwa na vikwazo fulani kwa kujumuishwa na kupata elimu ya kifedha. Wasichana hawana uhuru wa kifedha, lakini wanatarajiwa kuchangia mapato kwa kaya (Baraza la Idadi ya Watu 2012)
- Mara nyingi vijana wa kike wanakabiliwa na ubaguzi kwa njia ambazo zinaweza kuwathiri kupata elimu ya kifedha. Kwa mfano, mwanamke mmoja katika ya watatu hawana stadi za msingi za kuandika, na viwango vya usajili wa sekondari na masomo ya ziada kwa wanawake umepungua kuliko wanaume (UNESCO)
- Vijana wa kike wana wanakosa ajira kuliko wanaume; na kufanya kazi katika uchumi usio rasmi; na kutolipwa kwa kazi wanayoitoa (Restless Development; (Youthstart 2016)
- Kupata elimu na uwezo wa kujitegemea kifedha inaweza kusaidia vijana wa kike kupunguza kuwa katika hali hatarishi za kuwa katika umaskini, matatizo ya afya, ugomvi wa kijinsia na unyanyasaji ambao huwa na madhara kwa maisha yao na watoto wao kwa muda mrefu maishani (Population Council 2012)

BAADHI YA MASWALI KUHUSU JINSIA NA ELIMU YA KIFEDHA

Je, unaona kama jinsia ina atharisha upatikanaji wa elimu ya kifedha katika jamii yako?

_____

Je, unadhani vijana wa kike wamewezeshwa au hawana uwezo wa kifedha katika jamii yako?

_____

Je, unafikiria kuwa na elimu ya kifedha kunaweza kufanya tofauti katika maisha ya wasichana na wanawake wadogo katika jamii yako? Vipi?

MASUALA MUHIMU YA KUCHUNGUZA ZAIDI

- **Nafasi**: Takriban 60% ya vijana Tanzania wanaishi katika maeneo ya vijijini ambako fursa za ajira mara nyingi ni chache na kiwango cha umaskini kiko juu. Kilimo ni chanzo kikubwa cha ajira kwa vijana, lakini malipo ya kifedha kwa wanaotumia mbinu za zamani za kilimo yanaweza kuwa kidogo, na kulazimisha vijana kuongeza kipato chao kupitia shughuli zingine. Ujasiriamali katika minyororo ya thamani ya kilimo na chakula inatazamiwa na serikali, mashirika yasiyo ya mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi kuwa njia mojawapo iliyo na uhakika mkubwa kwa vijana kushiriki katika uchumi.

Maswali: Je, unaona fursa na nafasi katika kilimo na minyororo ya kuongeza thamani kwa bidhaa za chakula katika jamii yako? Ni nani wanaopata fursa hizi? Ni nini motisha na vikwazo vya kuanzisha biashara yako mwenyewe ya kilimo?

- **Teknolojia**: Huduma za fedha kupitia simu fedha zimebadili mazingira ya fedha ya Tanzania, na kurahisishia ubadilishanaji wa fedha katika maeneo ya vijijini na katika sekta isiyo rasmi. Nusu ya watu wazima nchini Tanzania walikuwa na akaunti ya simu mwaka wa 2014, na kufikia mwaka 2016 theluthi mbili ya watu wazima walijisajilisha kuwa na akaunti ya simu (InterMedia 2016)

Maswali: Je, huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zimebadilisha vipi maisha katika jumuiya yako kivipi? Kuna fursa mpya ambazo zinajitokeza kwa vijana kutokana na kuenea kwa huduma za kifedha za simu (mobile money)?

- **Ustawi**: Haihusiani tu na utajiri wa mali au pesa ulizonazo kwenye accounti yako ya benki. Kujifunza jinsi ya kusimamia fedha zako pia kunaweza kuchangia kujiheshimu na kuboresha ustawi wako, utambulisho na malengo yako (Population Council, Taking Stock)

Maswali: Unahisi vipi kuhusu hali yako ya kifedha? Unahangaika kuhusu pesa? Una wasiwasi upi haswa? Je, wewe na marafiki wako mnazungumzia pesa? Hali yako ya kifedha inathiri furaha yako, jinsi unavyohisi na kujtazama mwenyewe kivipi?

NYENZO YA RASILIMALI ENDELEZA UTAFITI WAKO!

- https://www.youtube.com/watch?v=jOwi8sAAzEA
- Jinsi Teknolojia inaendesha kuingizwa kwa kifedha Afrika (video kutoka CNBC / Mastercard kutoka WEF 2017)
- Makundi yasio rasmi ya kutunza pesa na kujumuisha watu kifedha nchini Rwanda
- Repoti ya African Development Bank ya kujumuisha watu kifedha (2013)
- Video 13 za IFC kuhusu mada ya kujumuisha watu kifedha Africa
- Kufungua njia za biashara kupitia vijana Afrika
- Makundi ya hifadhi isiyo rasmi na kuingizwa kwa kifedha nchini Rwanda
- Ripoti ya kuingizwa kwa kifedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (2013
- Mfululizo wa IFC wa video fupi 13 za kuingiza fedha katika Afrika
- Kufungua biashara ya kifedha kupitia vijana wa Afrika

UTANGULIZI KWA ELIMU
YA KIFEDHA

MWONGOZO WA KUTAYARISHA KIPINDI CHA REDIO

MWONGOZO WA KUTAYARISHA KIPINDI CHA REDIO

UTANGULIZI KWA ELIMU YA KIFEDHA

MAANDALIZI YA KIPINDI

NJIA YA KUZUNGUMZIA NA KUELEWA MAZINGIRA YA KIFEDHA KATIKA JUMUIYA YANGU

- Ni nani anayeshiriki katika mtiririko wa pesa katika jumuiya yako? Kivipi?
- Je, vijana hushiriki kivipi katika mtiririko wa pesa katika jumuiya yako?
- Vijana wana matarajio gani ya kifedha katika jamii yako?
- Je, watu hujiwekea malengo ya kifedha?
- Ni malengo gani ambayo ni ya muhimu kwa watu?
- Ni nini kinachofanya watu kusikia wanaweza kufanikiwa (au kutofanikiwa) kufikia malengo yao ya kifedha?
- Je, watu huweka akiba katika jumuiya yako? Nini husababisha watu kuweka akiba ?
- Je, watu huweka akiba kibinafsi au kama familia? Watu hutumia hizo akiba za pesa kwa matumizi yapi? Ni nani anayeamua?
- Ni nani katika jumuiya yako anayeonyesha mfano mzuri wa kukopa, kuweka akiba na kuwekeza pesa?
- Ni rasilimali na fursa zipi zilizopo katika jumuiya yako za kujifunza kuhusu fedha?

Njia tofauti za kuzungumzia elimu ya kifedha

- Kuelewa mazingira ya kifedha katika jumuiya yangu
- Ujumuishwaji wa kifedha na ajira kwa vijana nchini Tanzania
- Jukumu la vijana nchini Tanzania katika mambo ya kifedha kwa siku zijazo
- Jinsia inavyo athiri elimu ya kifedha na upatikanaji wa pesa

CHAGUA MADA MAHUSUSI

Kuelewa mazingira ya kifedha katika jumuiya yangu

MIUNDO YA REDIO

SAUTI YA UMMA

Lengo la sauti ya umma
Kupata maoni mengi juu ya mada moja.

Ni na nani unayezungumza naye
Mtu yeyote kutoka kwa jamii

Swali
Je, elimu ya kifedha ni nini?

MAONI YA SAUTI

Maoni ya sauti yanalenga
Kupata maoni ya watu juu ya mada ambayo wanayoijali sana.

Utazungumza na nani
Muulize kijana ambaye ana matarajio na matumanini ya kifedha na ni muwazi kuzungumzia juu ya mipango yake ya kifedha

WASIFU WA SAUTI

Lengo la wasifu wa sauti
Kupata masimulizi ya mtu aliye na uzoefu au shauku katika jambo fulani. Mara nyingi muundo wa audio profile unatumika kwa kuhamasisha wengine.

Utazungumza na nani
Mtaalamu wa kifedha au mmiliki wa biashara katika jumuiya ambaye anaweza kuzungumza juu ya safari yake ya kifedha, ikiwa ni pamoja na uzoefu wake wa kuweka malengo, bajeti, kuuchukua mkopo na kuweka pesa akiba.

Maswali ya kuuliza kabla ya kuanza kurekodi ili kumsaidia mhusika kufikiria wasifu au simulizi yake

- Je, unawezaje kuelezea maana ya elimu ya kifedha?
- Je, unaweza kutuelezea uelewa wako wa elimu ya kifedha wakati ulipoanza kusimamia fedha zako?
- Je, maarifa yako kuhusu fedha yamebadilika kivipi tangu wakati huo?
- Uliweza kupata rasilimali na fursa za kujifunza zaidi kuhusu fedha katika jumuiya? Hizo rasilimali na fursa zilikuwaje?
- Ni baadhi ya changamoto zipi ambazo umezipitia katika mikakati ya kusimamia fedha yako?
- Ni wapi ulipopata msaada wakati wa kukabiliana na changamoto hizo? (benki, mashirika, watu, nk)

TANGAZO LA UMMA

Kuweka mwamko wa jamii kuhusu jambo fulani.

Tumia ubunifu. Unaweza kuandaa tangazo lako la umma liwe kama mchezo wa kuigiza.

JINSI YA KUENDESHA KIPINDI

Tumia vipengele, utafiti wako, muongozo uliopendekezwa na maswali kuandika muongozo wako mwenyewe.

[KUFUNGUA KIPINDI:]
Mtangazaji 1: Imefikia saa [MUDA] na ni wakati wa [JINA LA KIPINDI] kwenye [JINA LA KITUA CHA REDIO]. Jina langu ni [JINA LAKO].

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [JINA LAKO]. Kipindi cha leo kitakuwa kuhusu elimu ya kifedha! Ndiyo, marafiki zangu, mmumesikia hiyo. Tutazungumzia jinsi sisi vijana tunavyoweza kuongeza ujuzi ili kusimamia fedha zetu na kuboresha ustawi wetu.

Mtangazaji 1: Hiyo ni kweli, tutazungumzia umuhimu wa vijana kkupata taarifa kuhusu jinsi tunaweza kufanya maamuzi sahihi wakati wa kusimamia fedha, akiba, mikopo, na mengine mengi. Huu ndio ukweli - Vijana nchini Tanzania ni karibu theluthi mbili ya idadi ya watu, na bado sisi tunahusishwa kwa nadra sana katika raslimali za ajira na misaada ya kifedha.

Mtangazaji 2: Leo hii, tutaangazia fursa za vijana za kifedha na rasilimali katika jumuiya zao wenyewe. Ili kufanya hivyo, vijana wanaweza kuanza kwa kutambua jinsi fedha na mzunguko wa fedha unavyofanya kazi katika maisha yetu ya kila siku. Sisi hapa tunakuletea taarifa za muhimu sana zinazohitajika zaidi ili kuanzisha mazungumzo ya wazi kuhusu ajira kwa vijana na ushirikishwaji wa kifedha!

Mtangazaji 1: Hebu tuanze kwa kusikia zaidi kuhusu kile ambacho watu wanafikiria kuhusu elimu ya kifedha na kujumuishwa kwa vijana.

[TAMBULISHA MGENI ANAYEHOJIWA]

[CHEZA MAHOJIANO]

[FUNGA KIPENGELE CHA MAHOJIANO]

[FUNGA KIPINDI]

Mtangazaji 1: Leo, tumejifunza mengi kuhusu elimu ya kifedha na vijana kupata rasilimali hizo!

Mtangazaji 2: Mtangazaji 2: Naam! Kuelewa pesa ni muhimu sana kwetu vijana ili kufanya maamuzi sahihi na mipango mizuri ya maisha yetu!

Mtangazaji 1: Wiki ijayo, siku ya [TAJA SIKU] saa [MUDA] tutazungumza kuhusu [TAJA MADA YA WIKI IJAYO]. Hadi wakati mwingine, kwaherini!

MUUNDO AU MPANGILIO WA KIPINDI



MAADILI NA IDHINI/ RIDHAA

Hakikisha umewafahamisha wasikilizaji kuwaheshimu wale wanaotoa hadithi zao za kibinafsi.

MPANGILIO WA SHUGHULI ZA KUFIKIA JAMII

Unapopanga shughuli yako ya kufikia jamii, tahadhari nishati ambayo shughuli
fulani huzalisha ili uepuke kuanza kwa kishindo na kisha kumalizia kwa wepesi.

UTANGULIZI KWA
ELIMU YA KIFEDHA

MUUNDO WA SHUGHULI YA KIJAMII

MUUNDO WA SHUGHULI YA KIJAMII

MZUNGUMZAJI MWALIKWA

Lengo la Mzungumzaji mwalikwa
Ni mtu ambaye anaweza kuelezea ujuzi wake wa kitaalamu au kutoa simulizi yake binafsi kuhusiana na mada.

- Je, elimu ya kifedha ni nini?
- Vijana wanaweza kunufaika vipi kwa kuelewa jinsi ya kusimamia pesa?
- Ni mabadiliko yapi makubwa ya kitabia ambayo vijana wa kitanzania wanahitaji kuyafanya kuhusiana na pesa?
- Ni vipi vijana wanaweza kuanza kuweka malengo na kuandaa mipango yao ya baadaye?

IMPACT JINGLE

Lengo la Impact Jingle
Jingle ni wimbo au kiashiria ambacho ni rahisi kuimba na kuukumbuka, na ina ujumbe ulio wazi, na unaoeleweka kirahisi.

MAHOJIANO

Lengo la mahojiano
Mahojiano ni mazungumzo ya watu wawili ambapo maswali yanaulizwa na mhojaji na majibu kutolewa na mhojiwa.

Suggested questions for an interview with a business owner in the community:
Maswali yaliyopendekezwa ya mahojiano na mmiliki wa biashara katika jumuiya:

- Je, elimu ya kifedha ina maana gani kwako?
- Je, unawezaje kueleza uelewa wako wa elimu ya kifedha wakati unapoanza kusimamia fedha zako ulikuwa vipi?
- Je, maarifa yako kuhusu fedha yamebadilika kivipi tangu wakati huo?
- Ulipata rasilimali na fursa za kujifunza zaidi kuhusu mambo ya kifedha katika jumuiya? Rasilimali na fursa hizi zilikuwaje?
- Ni baadhi ya changamoto zipi ulizokabiliana nazo katika juhudi zako za kusimamia fedha?
- Ni wapi (benki, mashirika, watu, nk) ulipopata msaada wakati wa kukabiliana na changamoto hizo?
- Ikiwa vijana wangetaka kujifunza na kuelimika kifedha zaidi, ungewaelekeza wapi?

KUIGIZA

Kutoa fursa ambayo inaruhusu washiriki “waigize” jambo kuhusu sentensi ya matokeo.
Amua wahusika wanaohitajika watakuwa wangapi, kisha wape ‘waigizaji’ nafasi wajadili sentensi ya matokeo. Waachie waigizaji waigize na kuiunda wakiendeleza zoezi.

Funzo: Kuweka kiasi kidogo cha pesa pembeni mara kwa mara kunaweza kukusanya akiba ya mtu.

Waigizaji wahusika: Amina, Baba Amina (babake Amina), na Mjaka (rafiki wa Amina)

Hali:
Amina ana umri wa miaka 19 na amemaliza kidato cha sita mwaka jana. Anafanya shughuli ya kuuza mifuko ya plastic kwa wauza matunda na wauza mboga katika soko la mtaani na hupata faida ya wastani wa Tshs 5,000 kwa wiki. Huchangia nusu ya pesa zake (Tshs 2,500) katika familia yao kwa ajili ya chakula. Na hutumia pesa zingine Tshs 2,500 kwa ajili ya kununua nguo za kisasa na kula bata mwisho mwa wiki (wikendi) na rafiki yake wa karibu sana aitwaye Mjaka.

Baba yake Amina lipoteza kazi katika kiwanda cha mtaani miezi nane iliyopita, na tangu kipindi hicho mpaka sasa bado hajapata ajira. Hivi karibuni alimwambia Amina kuwa kwa sababu yeye (baba) hana kipato chochote anachoingiza wala akiba yeyote ile itakuwa ngumu kupata fedha za kumsaidia Amina kutimiza ndoto yake ya kujiunga na chuo mwaka ujajo.

Amina ana dhamira ya kwenda kusoma chuo lakini hana uhakika wa kuweza kukusanya pesa kwa ajili ya ada ya shule.
Unawezaje kumshauri Amina?

MJADALA WA JOPO

Mjadala wa jopo
Mjadala wa jopo unahusisha kundi la watu wakijadili mada moja mbele ya watazamaji.
Kwa kawaida, mwisho kuna fursa ya maswali kutoka kwa watazamaji.

Ni nani anahusika kwa jopo
Wataalam wa kifedha na washauri (pamoja na utaalamu tofauti wa kuweka pesa akiba, mipango ya kifehda, mikopo na uwekezaji), vijana wenye matarajio ya kifedha, wazazi.

Mifano ya maswali ya kufungua jopo

- Kwa nini ni muhimu kwa vijana kuelewa pesa na jinsi inavyofanya kazi?
- Kwanini ni muhimu kuweka akiba ya pesa (kutunza)?
- Je, mtu aliye na mapato ya chini au yasiyo ya kutegemea anaweza kuweka pesa akiba pia? Ikiwa ndivyo, kwa jinsi gani?
- Kuna wakati maalum kwa vijana kuanza (au kuacha) kuweka abika?
- Je, watoto na vijana wanapaswa kushirikishwa katika majadiliano kuhusu maamuzi ya kifedha ya familia?
- Ni wapi katika jumuiya ambapo vijana wanaweza kupata elimu na taarifa na msaada zaidi wa mipango yao ya kifedha?
- Je, vijana wanahitaji kuelewa nini kuhusu kukopa na kukopesha? Mikopo hufanyika kivipi?
- Ni faida na athari zipi zilizopo kwa kukopa na kukopesha pesa?
- Ni wapi katika jamii ambapo vijana wanaweza kupata elimu na taarifa zaidi juu ya kukopa na kukopesha pesa?

JINSI YA KUANDAA SHUGHULI YAKO YA KIJAMII

Tumia vipengele vya shughuli ya kijamii yako na utafiti wako kuandika muongozo wako.. Hapa kuna mfano wa sehemu ya muongozo. Tumia huo muongozo wako kupanga shughuli yako ya kijamii sasa.

Maswali yaliyopendekezwa kwa mahojiano yako na mmiliki wa biashara katika jumuiya.

- Elimu ya kifedha ina maana gani kwako?
- Je, unawezaje kuelezea uelewa wako wa elimu ya kifedha wakati ulipoanza kusimamia fedha zako?
- Je, maarifa yako kuhusu fedha yamebadilika kivipi tangu wakati huo?
- Upata rasilimali na fursa za kujifunza zaidi kuhusu fedha katika jumuiya yako? Hizo rasilimali na fursa zilikuwaje?
- Ni changamoto zipi ulizokabiliana nazo katika juhudi zako za kusimamia fedha?
- Ni wapi (benki, mashirika, watu) ulipata msaada wakati wa kukabiliana na changamoto hizo?
- Ikiwa vijana wanataka kujifunza zaidi kuhusu elimu ya kifedha , utawaelekeza wapi?

[FUNUGA KIPENGELE CHA MGENI MZUNGUMZAJI]

Mtangazaji 1: Hamjambo na karibuni! Imefikia [SAA] na jina langu ni [JINA LA MTANGAZAJI 1] na mimi ni [SIFA AU JUKUMU] kutoka [JINA LA SHIRIKA]. Leo tunaangazia swala muhimu ambalo limetuathiri sote kwa njia moja au nyingine.

Mtangazaji 2: Na jina langu ni [JINA], mimi ni [SIFA AU JUKUMU] kutoka [JINA LA SHIRIKA] na kipindi cha leo ni kuhusu jinsi vijana tunaweza kupata rasilimali na kuboresha ujuzi wetu wa kusimamia fedha zetu na ustawi wetu kwa ujumla.

Mtangazaji 1: Hivyo ndivyo ilivyo! Tutazungumza juu ya umuhimu wa vijana kupata elimu ya kifedha ili kuelewa kufanya maamuzi mazuri wanaposimamia pesa, akiba, mikopo, na mengine mengi zaidi. Ukweli wa mambo ni kwamba vijana wamekaribia kufikia theluthi mbili ya idadi ya watu nchini Tanzania, na bado sisi hatuhusishwi katika rasilimali za kifedha na ajira.

Mtangazaji 2: Yeah, na ndio sababu tutakuwa tunaangazia vijana kupata fursa za kifedha na rasilimali katika jamii zao. Ili tuweze kufanya hivyo, vijana wanaweza kuanza kwa kutambua jinsi fedha na mtiririko wa pesa hufanyika kwa maisha yetu ya kawaida. Na ndio maana nasi tunakuleta taarifa zinazohitajika kuanzisha mazungumzo na majadiliano ya wazi kuhusu elimu ya kifedha na kujumuishwa kwa vijana!

Mtangazaji 1: Hebu tusikie zaidi kuhusu kile ambacho watu wanasema kuhusu elimu ya kifedha na kujumuishwa.

[FUNGUA MAHOJIANO]

[MAHOJIANO]

[FUNGA MAHOJIANO]

Mtangazaji 1: Wow! Hiyo ilikuwa taarifa ya kuhamasisha sana! Kuna mambo mengi kuhusu kusimamia pesa na kupata rasilimali zaidi ya unavyoweza kufikiria.

Mtangazaji 2: Kweli kabisa! Sisi, kama vijana, tuna haki ya kupata maelezo ambayo yanaweza kutunufaisha na kuboresha ustawi wetu wa sasa, na siku zijazo. Hebu tafakari maisha yako wewe ukiwa na uelewa na ujuzi wa kusimamia akiba, mikopo, na mengi zaidi!

Mtangazaji 1: Kweli hapo umenena! Sasa hebu tupate maelezo zaidi kutoka kwa mgeni wetu leo ambaye ni mtaalamu wa kifedha. Yeye atatusaidia kuelewa zaidi kuhusu elimu ya kifedha. Pia baadaye, tutakuwa na maswali kupitia kwizi (maswali ya papo kwa papo) yetu, na tutaangazia maana ya Kujumuishwa Kifedha, na mengi zaidi! Usibanduke hapo ulipo!

[FUNGUA KIPENGELE CHA]

[MGENI MZUNGAMZAJI]

JINSI YA KUANDAA SHUGHULI YAKO YA KIJAMII

Tumia vipengele vya outreach yako na utafiti wako kuandika muongozo wako.. Hapa kuna mfano wa sehemu ya muongozo. Tumia huo muongozo wako kupanga shughuli yako ya kijamii sasa.

Maswali ya mahojiano yako na mshauri au mtaalam wa kifedha

- Elimu ya kifedha ni nini?
- Kujumuishwa kifedha ina maana gani?
- Je kuna athari gani kutokana na kutoele-wa mambo ya kifedha?
- Elimu, rasilimali na fursa za kifedha zinaweza kufanywaje ili kupatikana kwa urahisi zaidi kwa vijana?
- Ni hatua zipi ambazo wewe ungepend-ekezavijana walio na ndoto an matarajio za kifedha kuchukua?
- Vijana wengi Tanzania wanafanya kazi katika sekta isiyo rasmi, na hawana mikataba ya ajira au nyaraka za ushahidi wa malipo (payslip). Wanaweza aje basi kupata huduma bora zaidi za kifedha?

[JE KUNA ATHARI GANI KUTOKANA NA KUTOELEWA MAMBO YA KIFEDHA?]

[CHEZA JINGLE]

Mtangazaji 1: Tumejifunza mengi kutoka katika mahojiano na mgeni wetu. Sasa hebu tusikie kutoka kwako kupititia mchezo wa quiz fupi. Hivi ndivo quiz itakavyokuwa

[FUNGUA NA KANUNI ZA QUIZ]

[FANYA KWIZI YA KUPIMA MAARIFA NA UELEWA] Unaweza kuunda moja kwa kuuliza maswali kuhusu elimu iliyoenezwa kupitia outreach AU kwa kuangalia ujumbe uliopo katika sehemu za “Ukweli na Fikira au Taarifa Potofu ” na “ Ujijua Kwamba”.

[FUNGA QUIZ]
[CHEZA JINGLE]

[Hapa, endelea na muongozo wako kulingana na muundo wa outreach yako hapa chini]

[FUNGA KIPENGELE CHA QUIZ]
]

Mtangazaji 1: Leo, tumejifunza mengi kuhusu elimu ya kifedha na kujumuishwa kwa vijana!

Mtangazaji 2: Ndiyo, ni vizuri tumeelimika na kujua kwamba kusimamia pesa haihusiani tu na kununua vitu, lakini pia inahusu kujiwekea malengo na mipango kwa ajili ya siku zijazo!

Mtangazaji 1: Kweli! Elimu ya kifedha inahusu kufanya maamuzi mazuri ili kuboresha maisha yetu. Usisahau kujiunga nasi mwezi ujao tarehe[SIKU NA TAREHE] saa [MUDA] kwenye [WAPI]. Tutazungumzia [TAJA MADA YA KIPINDI KITAKACHOKUJA]. Asante kwa kujiunga nasi! Ni matumaini yetu kwamba utajiunga nasi tena wakati mwingine!

Mtangazaji 2: Hadi wakati huo, kutoka kwetu tunakuaga kwaherii!

MUUNDO AU MPANGILIO WA SHUGHULI YA KIJAMII

Muundo wa shughuli ya kijamii ni mpangilio ambao utakaokusaidia kuendelea kuwa katika mstari sahihi wakati wa shughuli yako. Ni orodha na mpangilio wa mambo yatakavyofuatana kwenye shughuli yako ya kijamii.

Ufuatao hapo chini ni mfano wa muundo wa shughuli ya kijamii ya saa moja:



MAADILI NA RIDHAA

Hii inaweza kuwa mada nyeti kwa baadhi ya watu, kwa hivyo hakikisha umewajulisha washiriki wako kuheshimu wale watakaosimulia hadithi zao za kibinafsi katika wasaa hii.

Kama taarifa yoyote isiyo sahihi itajitokeza popote katika moja ya vipengele vyako kama vile kwizi, igizo au jopo mjadala, ni lazima kuisahihisha. Usiache watazamaji wako waondoke na taarifa potofu. Pindi unapokuwa umemaliza muongozo wako, mpangilio wa wasanii wako wa kutumbuiza, vipengele tofauti na muundo wa shughuli yako ya kijamii, basi uko tayari kuanza shughuli yako mbashara!